

## Mitandao ya Kijamii na Mabadiliko ya Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja

*Kenyani Sangili*  
*Chuo Kikuu cha Rongo*

### **Ikisiri**

Wanafalsafa wa kale walidai kuwa, duniani, hakuna kitu ambacho hakikosi kubadilika. Mojawapo ya vitu vinavyobadilika ni lugha. Lugha za binadamu hubadilika katika kila kizazi kwa sababu mbalimbali za kiisimujamii na kiteknolojia. Kwa kuwa lugha za binadamu ni kitu changamano, mabadiliko yake hutokea kwa matawi ya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kisemantiki na kipragmatiki. Kuna sauti ambazo hutoweka katika lugha, na zingine hukopwa. Maana za leksimu hupanuka au hufinyika kutegemea matumizi yake kimuktadha. Kwa njia hii, mawasiliano ya binadamu huathirika kwani mabadiliko ya lugha hubadilisha mawasiliano na jinsi washiriki wanavyofasiri maana za kauli. Utafiti huu ulichunguza mabadiliko ya lugha ya Kiswahili mintarafu mitandao ya kijamii. Hii ni kwa sababu mojawapo ya vitu vinavyosababisha lugha kubadilika katika karne ya 21 ni teknolojia.

**Maneno Muhimu:** *Mabadiliko ya Lugha, Kijamii, Mtandao*

### **Utangulizi**

Mabadiliko ni dhana inayojikariri kila mara katika shughuli zote za binadamu na viumbe wengine. Watoto hubadilika kwa kukua kufikia utu uzima na mimea hubadilika kwa kuzalisha matunda na majani. Wanavyosema wanafalsafa wengi kama vile Heraclitus, Edmund Spenser na Von Humboldt, mabadiliko ni kitu kisichoepukika, hasa mabadiliko ya lugha (Aitchson, 2001). Lugha za binadamu zinachukua mikondo na mielekeo mipya kila kizazi kwa kulenga matumizi na ufaafu wa kijamii. Lugha za kale kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani na Kiswahili ni muhali kueleweka zinapotumika katika kizazi cha leo. Hii ni kwa sababu, zimepoteza baadhi ya maneno, zimepanuka kimaana, zimedhalilishwa kimaana, na vilevile, sauti za baadhi ya maneno zimetoweka au zingine kuongezwa kutokana na mtagusano au usahilishaji wa matamshi (Strazny na Trask, 2000; Lewis, 2009). Katika taaluma ya Kiswahili, na hususan ushairi wa jadi wa Kiswahili, leksimu nyingi ni ngeni kwa wasomaji wa leo kwa sababu baadhi ya maneno yaliyotumika ni mageni kwao, yamebadilika kitabdila au sauti zimedondoshwa kabisa. Baadhi ya maneno haya yamechambuliwa kutoka tenzi mbalimbali na mashairi ya Kiswahili ya kabla ya karne ya 20 (Shitemi, 2010).

Kwa mujibu wa Breivik na Jahr (1989), lugha zinabadilika ili kutosheleza mahitaji ya mawasiliano ya kipindi fulani. Huenda tunashuhudia mabadiliko ya mnyonge msonge na mwenye nguvu mpishe, kwa maana kuwa, mabadiliko yenye nguvu kuu kiuamilifu ndiyo yanakubalika huku yale yaliyo dhaifu yakipotea baada ya msimu. Katika jamii za leo, wanajamii wengi wamesoma lugha na sheria zake katika mifumo mbalimbali ya shule. Hata hivyo, badala ya wao kuzitumia sheria hizi, wanazikaidi katika kile ambacho Jahr (1998) anataja kama “kuchezea lugha ili kutimiza mahitaji na stadi”. Kwa mujibu wa wanasarufi elekezi, baadhi ya wanajamii hawa hawana haja ya kuzingatia sheria za lugha kama zinavyotambulishwa na watu fulani katika jamii-lugha. Wao huona kwamba, wanapowekewa sheria za kufuata katika mawasiliano kisarufi, wanakosa uhuru wa kujieleza ipasavyo. Ndiposa Mohamed (2002) anazungumzia dhana ya kukaidi sheria katika shairi ‘Arudhi’. Anadai kuwa:

Kina, cha nini kina?  
Kina, sitaki kina- iwapo chalazimishwa:  
la kije kwa hiari  
tena kije vizuri  
kilingane na pumzi (2002 : 78)

Kukaidi sheria za utunzi wa mashairi ya Kiswahili ndiko kulizalisha mashairi ya kisasa/kimapinduzi. Vivyo hivyo, kukaidi sheria za kiisimu ndiko huzalisha mabadiliko ya lugha miongoni mwa watumiaji wake. Mifumo mipya ya kileksimu tunayoshuhudia katika Isimu-historia imetokana na wanajamii wenyewe kukaidi sheria mahsusi zinazotawala urasimi wa mifumo ya kiisimu. Lengo kubwa la kukaidi sheria hizi zinatokana na mwanajamii kupata uwezo na uhuru wa kujieleza bila vikwazo vyovyote vya kiisimu au kiarudhi. Watumiaji lugha hufuata maelezo ya wanasarufi fafanuzi wanaosema kuwa katika lugha, kile ambacho ni muhimu katika uchanganuzi ni kile kinachosemwa na watu. Kanuni hizi si za kidhahania bali zinatokana na jinsi lugha hiyo inavyosemwa. Kwa mfano, katika Kiswahili, uunganishaji wa sauti ili kuunda maneno hufuata sheria maalumu kama vile: [K+I, K+I+K+I]. Kwa mfano sauti hizi ni za Kiswahili na zinapounganishwa, zinazalisha maneno ya Kiswahili kwa jinsi hii :

/a/, /a/, /ch/	=	[acha] na wala siyo
	=	[aach]
/a/, /a/, /p/	=	[paa]
	=	[apa] na wala siyo
	=	[aap]

Kimsingi, maneno ya Kiswahili hayaishii kwa konsonanti, hivyo, ikiwa itatokea kinyume na sheria hii, na kinyume hiki kivumishwe kiuamilifu, basi hali hii husababisha badiliko fulani katika lugha. Sheria hizi hutawala pia kiwango cha mofolojia, hasa katika viambatishi na vinyambuo vya Kiswahili.

### **Vipengele vinavyobadilika katika Lugha**

Tunaposema kwamba lugha za binadamu zinabadilika, tunamaanisha nini hasa? Ni vipengele vipi ambavyo vinastahili kuchunguzwa ili kuthibitisha kwamba lugha imebadilika? Kulingana na watafiti mbalimbali, lugha hubadilika kwa ujumla, yaani, kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kisemantiki na kipragmatiki (Hickey, 2001; Mey, 2009; Androupoulos, 2011). Kwa hiyo, katika kurejelea utafiti unaohusu mabadiliko ya lugha, pana haja ya kuchunguza vipengele hivi kama vinavyodhihirisha mabadiliko wakati fulani.

Lugha hubadilika kwa sababu mbalimbali kama wanavyofafanua wataalamu wengi. Mey (2009) anadai kwamba lugha za binadamu zinabadilika kwa sababu utamaduni unaoambatana na lugha hizi unabadilika. Kwa kuwa lugha na utamaduni ni vitu viwili visivyoweza kutenganishwa, kimoja kinapobadilika, chenzake pia hubadilika. Utamaduni ni dhana pana kwani inahusisha vipengele vingi kama vile tabia za watu wa jamii moja, mapendeleo yao kijamii, na jinsi ya kujieleza au kuelezea dhana mbalimbali zinazowatawala (Wardhaugh, 2002). Elmes (2013) anadai kwamba utamaduni hudumishwa na kuwasilishwa kupitia lugha. Lugha nayo hudumishwa kupitia utamaduni. Kunapotokea upya katika utamaduni, basi hali hii husababisha uzalishaji, ukopaji na ubunaji wa msamiati mpya unaoelezea tukio au dhana hiyo mpya. Kwa mfano, kwa kuwa jamii za Afrika Mashariki zimeingiza teknolojia katika utamaduni wake, hali hii imepelekea ubunaji wa msamiati mpya na kubadilisha Kiswahili kwa kuiongezea maneno mapya. Maneno haya yameingizwa katika Kiswahili kupitia njia mbalimbali kama vile ubunaji, ukopaji, na upanujaji kimaana na kimatumizi, kama mifano ifuatayo inavyoonyesha.

Diskimweko/Kinyonyi – *Flashdisk*  
King'amuzi- *Decoder*  
Kiwambo- *Monitor*

Jumla ya maneno haya yanaelezea upya ulioingizwa katika utamaduni wa jamii za Afrika Mashariki, na hivyo, palitokea haja ya kubuni au kupanua istilahi zilizokuwepo kuelezea upya huu. Kiswahili hiki kinapolinganishwa na Kiswahili cha kale ambacho ni Kingozi, basi ni bayana kwamba baadhi ya maneno haya hayakuwepo, na kama yalikuwepo, hayakuwa na fahiwa hizi mpya za kiteknolojia.

Sababu ya pili ya kubadilika kwa lugha ni upashanaji wa lugha kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Tafiti zimeonyesha kwamba njia ya pekee ya kudumisha lugha ni kupitia kwa kizazi kimoja hadi kingine (Crystal, 2003). Ikiwa lugha itakufa au kutoweka, basi ni dhahiri kwamba, ilikosa wasemaji, hasa kizazi kichanga kilichostahili kuiendeleza mintarafu ya shughuli zao za kila siku. Mara nyingi, vipengele vya lugha vinapopitia kizazi baada ya kingine, husababisha mabadiliko ya sauti, msamiati, maana na matumizi ya maneno (Hickey, 2001). Baadhi ya sauti hutoweka au kupitia hatua za ukaakaishaji, usimilishwaji na michakato mingine (Mgullu, 1999; Obuchi na Mukhwana, 2015). Vilevile, kuna uwezekano wa vizazi fulani kuhamahama na kujikuta katika mazingira mapya ya kiisimu, misamiati

mipya hukopwa kutoka kwa lugha hizi ngeni. Misamiati hii husimilishwa katika lugha na kuwa sehemu ya hazina mpya. Baadhi ya maneno huchukua maana mpya au kufinyika kimaana. Maana inapopanuka, husababisha ung'amuzi wa wanajamii kupanua kamusi ya akili zao ili kuhusisha maana hizi mpya. Kwa mfano, katika mawasiliano miongoni mwa baadhi ya wanajamii nchini Kenya, maneno haya yamepanuliwa kimaana na kizazi cha vijana:

Neno	Maana ya kawaida	Maana iliyopanuliwa
Mbuyu	aina fulani ya mti	baba mzazi mwanamume mzee
Bamba	kipande cha bati	kushika; kufurahisha
Missed call	simu ambayo haikupokelewa	mtu aliyeadamika
Mteja	mnunuzi wa bidhaa	mtu aliyeadamika sana
Choma	kutia kitu moto	kuendesha gari kwa kasi
Bonga Points	Jumla ya alama ambazo mtumiaji wa mtandao wa saraficom hutuzwa anapotumia tasnia zake	Sehemu za nyuma za mtu/ makalio/matako ya binadamu

Jedwali hili linadhihirisha jinsi maana na matumizi ya maneno katika lugha hubadilika kwa kupanuka kisemantiki na kipragmatiki kutegemea kizazi baada ya kizazi.

Sababu nyingine ambayo hupelekea lugha kubadilika ni ubunifu wa watumiaji wake. Baadhi ya wanajamii hupenda kubuni maneno kuelezea kadhia au matukio katika ulimwengu wao. Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa msamiati unaobuniwa hauna visawe vyake katika lugha husika. Wabunaji huumba msamiati kwa lengo la kufanikisha mawasiliano, na mchakato huu hutegemea umri, elimu, taaluma na muktadha. Baadhi ya watunzi wa mashairi na nathari hupenda kubuni maneno ambayo yatawasaidia kutosheleza mahitaji ya kishairi kama vile urari wa vina na mizani, upashaji wa maana kwa mtindo maalumu na hadhira wanayoilenga. Kwa mfano, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, mtunzi Said A. Mohamed amebuni maneno kama vile:

Nywelemaiti	- wig
Mfuhai/maitikwenda	- the living dead
Kimvumeme	- hairdryer
Wenyelsingazao	- those with natural sleek hair
Kurongofywa	- kudanganya
Waduhushibustani	- gardeners
Watamaduniwapya	- modernists
Kizamoto	- dark red (Bertoncini, 2002)

Ikiwa maneno haya yanapata mashiko na kusambaa miongoni mwa watumiaji wake, kunatokea uwezekano wa lugha husika kubadilika (Milroy na Milroy, 1985).

Kwa kweli, mabadiliko ya lugha, mara nyingi, huanzishwa na watu wa chini kitabaka kwani umilisi wao wa lugha huwa mbovu na pengine, duni. Na kwa kuwa wanalenga kujiwasilisha kikamilifu, hulazimika kubuni maneno mapya kujitosheleza. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba tabaka la juu haliwezi kusababisha mabadiliko ya lugha kwa kuvumbua istilahi mpya kuelezea shani fulani katika jamii. Kulingana na Aitchison (2001), mabadiliko ya sheria za lugha ya Kiingereza miaka ya 1755 yalifanywa na tabaka la juu kwa kuzingatia uamilifu wa lugha miongoni mwa wasemaji wa tabaka hilo.

Sababu ya nne inayopelekea lugha kubadilika ni mtagusano wa lugha mbalimbali. Wanajamii hutagusana na kila wanapokutana, huzalisha msamiati na sauti mpya. Kwa kuwa mazingira ambamo wanakutana ni ya wingilugha, hulazimika kutafuta mwafaka wa lugha ili kukamilisha mawasiliano yao. Mara nyingi, mazingira haya huzalisha Lingua Franca, Krioli na Pijini ambazo ni lugha zinazotumika na watu wenye lugha tofautitofauti. Maneno ya Kilingua Franca hukopwa na kuingizwa katika lugha, hivyo kuibadilisha. Trudgil (1989) anataja mbinu ya urahisishaji kama mojawapo ya njia za kuzalisha maneno mapya katika mazingira kama haya. Aitchison (2001) anadai kwamba lugha zinapokutana katika mazingira ya wingilugha, mojawapo ya lugha huweza kukopa maneno mengi na hata vipengele vya kisarufi ili kujiendeleza. Njia hii ya ukopaji wa misamiati kutoka lugha moja hadi nyingine inadhaniwa kuwa sababu kuu ya ubadilikaji wa lugha (Trask, 1994). Kwa mfano, lugha ya Kiingereza imewanda na kupanuka kimatuzi, kimsamiati na kimaana kwa sababu imekopa maneno kutoka kwa lugha zote ambazo inatagusana nazo. Baadhi ya maneno ni ya Kifaransa, Kijerumani, Kiswahili na Kijapani miongoni mwa lugha nyinginezo. Aidha, Kiswahili kimekopa maneno mengi kutoka Kiarabu, Kireno, Kiingereza, Kijerumani, Kihehe, miongoni mwa lugha nyinginezo za Kilimwengu na kiasili (Chiraghdin na Mnyampala, 1977). Ingawa maneno yanayokopwa yanakipanua Kiswahili, hatima ni kwamba, ukopaji huu unakisababisha mabadiliko ya lugha ya Kiswahili.

Sababu nyengine ambayo hubadilisha lugha ni teknolojia. Kuzuka kwa TEHAMA<sup>1</sup> katika maisha ya kila siku ya wanadamu yamebadilisha sana lugha. Kwa mujibu wa Androutsopoulos (2011) teknolojia imezalisha vifupisho kama vile *LOL*, *LOLMAO*, *FYI*, *WTF* ambavyo vinatumika tu katika mtandao wa kijamii bila kujikariri katika usemi wa kawaida. Hata hivyo, ifahamike kwamba, unaposikiliza maongezi ya vijana wa mijini na Vyuho Vikuu, baadhi yao hutaja vifupishi hivi; kwa mfano, wanapochekekana, mmoja anaweza kusema “LOL!” kumaanisha kwamba amefurahia kisemwacho. Vifupisho hivi, hata hivyo, havidumu sana kwani ni matukio ya msimu tu. Vilevile, kuwepo kwa mitandao ya kijamii na zana za kusakura kama vile blogu, *google*, *twitter* na *facebook* imesababisha upya wa

---

<sup>1</sup> TEHAMA- Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

istilahi za Kiingereza kama vile *blogaholic*, *ergoogeln*, *ergooglt*, *defriend*, *unfriend*, *befriend*, *facebook stalking*, *poke*, *tweet* miongoni mwa maneno mengine. Baadhi ya maneno haya yamekuwepo katika lugha ya Kiingereza ila yamepanuliwa maana. Maneno haya yameanza kupanuliwa kimatumizi kutoka kwa matumizi kimtandao hadi katika usemi wa kawaida. Kizazi kinachotumia maneno haya katika mazungumzo husema, kwa mfano, “I will *unfriend* you *ASAP*” kwa maana ya “urafiki wetu utakwisha mara moja hii.”

Mabadiliko ya lugha husababisha mielekeo na maoni mbalimbali kutoka kwa wapenzi wa lugha na wanaopendekeza au kusababisha mabadiliko haya. Baadhi ya wanajamii hukemea mabadiliko haya ya lugha huku wakidai kwamba yanatokana na uzohali na mapuuzo kwa upande wa wabadilishaji (Aitchson, 2001). Kwa mfano, katika miaka ya 1960, baadhi ya Waingereza walianza kutambua mabadiliko katika lugha yao. Wapenzi wa lugha ya Kiingereza walianza kuyaandikia magazeti wakilalamika kuwa baadhi ya maneno yalikuwa yanachukua utamkaji na maana mpya ambayo haikuwa sahihi. Wapenzi hawa wa Kiingereza walidai kwamba lugha hii ilikuwa na sauti ambazo zilikuwa vigumu kutamkwa na wageni ila maana zake zilikuwa rahisi kujua. Wakati huo, walidai kwamba lugha hii imebadilika kiasi cha Waingereza wenyewe kushindwa kutamka na kufahamu maana za baadhi ya maneno (Aitchson, 2001). Kilichowasikitisha ni kwamba, waliokuwa wanabadilisha lugha hii hawakuwa wageni ila wazawa wenyewe. Mabadiliko haya yanaweza yakanasibishwa na mabadiliko kitabia ya kizazi hiki ambapo wazee wa kale wanateta ya kwamba tabia, mavazi, vyakula na dunia ya leo imebadilika na kuwa mbaya ikilinganishwa na wakati wao. Hata hivyo, Kizazi cha leo hakioni tatizo lililopo katika mabadiliko haya kwani wanaona kwamba yanawafaa zaidi na yanawatofautisha na wazee wao. Ajabu ni kwamba, vijana wa leo watakapokuwa wazee, miaka hamsini baadaye, watalalamika kwamba “dunia ya leo imeharibika na kubadilika sana”. Mabadiliko yanatokea ili kutosheleza mahitaji ya watumiaji wake katika kipindi fulani cha kihistoria.

### **Kitandazi na Mabadiliko ya Lugha ya Kiswahili katika Karne ya 21**

Sehemu hii inajadili data kutoka kwa kurasa mbalimbali za watumiaji wa kitandazi, huku tukijaribu kuangazia zaidi mabadiliko ya fonolojia na mofolojia ya maneno maalumu ya Kiswahili.

### **Mabadiliko ya Kifonolojia**

Mabadiliko ya kifonolojia hutokea pale ambapo wanajamii lugha hubadilisha umbo la neno kwa kuingiza au kudondoa sauti fulani kinyume na ilivyozoeleka. Mabadiliko ya kifonolojia yamevutia watafiti wengi wa isimu wakiwemo Bynon (1977), Bakari (1982), Crawley (1992) na wengine wengi. Sababu kuu ambayo inapelekea utafiti wa aina hii kuegemea sana fonolojia ni kwa kuwa ni vigumu sana kufahamu mabadiliko katika nyanja zingine za mfumo wa lugha pasi ya kuelewa mabadiliko ya sauti za kifonolojia. Mabadiliko ya lugha yanaathiri orodha ya sauti katika lugha na mofolojia, sintaksia na semantiki ya lugha. Utafiti huu umeonyesha

kwamba, wasemaji wa Kiswahili wanadhihirisha mabadiliko haya katika maandishi yao ya kitandazi:

### **Kudondosha baadhi ya Sauti**

Udondoshaji wa sauti huhusisha kutoa kipashio fulani, konsonanti au irabu kutoka mfumo maalum (Mgullu, 1996; Njogu na wenzake, 2007). Kulingana na watafiti hawa, udondoshaji ni wa aina tatu:

#### **a) Udondoshaji Mwanzo**

Udondoshaji mwanzo ni mchakato wa kubadilisha mfumo wa neno kwa kutoa/kung'oa sauti au foni inayotangulia katika neno. Katika utafiti wetu, tulitambua kwamba watumiaji wa Kitandazi hawakuonyesha mabadiliko haya katika matumizi yao. Hali hii, pengine ni nadra sana kudondosha sauti ya kwanza na neno na likabaki na maana inayohitajika au inayoeleweka.

#### **b) Udondoshaji Kati**

Udondoshaji kati ni mchakato wa kuunda mfumo mpya wa neno kwa kungo'a sauti au foni iliyoko baina ya sauti zingine katika neno. Kwa mfano, jedwali lifuatalo linadhihirisha mchakato huu vyema:

**Jedwali 1**

<b>Neno</b>	<b>Sauti iliyodondoshwa</b>	<b>Matokeo/mfumo mpya</b>
vizuri	/i/,/u/,/i/	vzr
Wewe	/e/,/e/	ww
yote	/o/	yte
muda	/u/	mda
mbona	/o/,/a/	mbn
baba	/a/	bba
nini	/i/,/i/	nn

Kutokana na data hii, ni dhahiri kwamba watumiaji wa kitandazi wanapenda kudondosha sauti mbalimbali zilizo katikati mwa neno au leksimu. Baadhi ya maneno kama vile [vizuri] yanapoteza zaidi ya sauti tatu huku maneno [wewe], [mbona] na [nini] yakipoteza sauti mbili kila neno. Aidha, ni wazi kwamba kutokana na data hii, wasemaji wamezoea kudondosha irabu huku konsonanti zikisalia zilivyo. Si rahisi kufahamu maana ya mifumo mipya ya maneno kwa jinsi ambavyo sauti nyingi zimedondoshwa, hivyo, inamlazimu msomaji ajifunge kwenye muktadha ambamo mabadiliko haya yanatokea. Hivyo, uhusiano wa maneno katika mchakato mzima wa uzalishaji maana na udumishaji mawasiliano kipragmatiki unaibuka kama kipengele muhimu tunapojadili mabadiliko ya lugha katika ulimwengu wa kimtandao.

### c) Udondoshaji Tamati

Haya ni mabadiliko ya kifonolojia ambapo sauti au fonimu iliyoko mwishoni mwa mfumo wa neno hutolewa na wanajamii. Sababu kubwa inayopelekea udondoshaji huu ni kwamba wanajamii wanatafuta umbo lililo zuri na rahisi kwao na linalowasilisha jumbe zao kamili. Baadhi ya wanajamii wanatoa sababu kwamba hawaoni haja ya kukamilisha neno lao ikiwa tarari wanaeleweka na wenzao. Kwa mfano jedwali hili linadhihirisha mabadiliko haya:

#### Jedwali 2

Neno	Sauti iliyodondoshwa	Matokeo/mfumo mpya
anafaidi	/i/	Anafaid
hayawezi	/i/	Hayawez
umeketi	/i/	umeket
jamani	/i/	jaman
wanawivu	/u/	wanawiv
naitabaki	/i/	naitabak

Mabadiliko haya yanatokea wakati ambapo wahusika wa mawasiliano ya kitandazi wanashindwa kumaliza neno au wanadondosha sauti iliyoko katikati mwa neno. Kutokana na data hii, ruwaza kadhaa zinajikariri:

- Sauti inayodondoshwa zaidi ni irabu /i/
- Maneno mengi yanadondosha sauti za mwisho au kati. Ni nadra sauti za mwanzo wa neno kudondoshwa.
- Fahiwa ya neno haibadiliki wala kutatiza uelewa wa wanaoshiriki mazungumzo ya kitandazi.
- Sauti zinazodondoshwa ni irabu kwa kuwa haziathiri maana ya neno ikilinganishwa na konsonanti. Hii ina maana kwamba uzito wa sauti unazingatiwa kabla ya kuchakata udondoshaji. Mchakato huu wa kuchagua sauti ya kudondosha ni wa king'amuzibwete zaidi.

Kutokana na mahojiano na baadhi ya watumiaji wa kitandazi, ilikuwa ni bayana kwamba washiriki hawakuonyesha tatizo kuhusiana na udondoshaji wa baadhi ya sauti. Waliekea kufahamu kile ambacho wenzao walikuwa wanadhamiria.

#### Uchopekaji, Uingizaji na Upoteaji wa Sauti

Uchopekaji au uingizaji wa sauti ni mchakato wa kubadilisha mfumo wa neno kwa kuingiza irabu au konsonanti katikati mwa mfumo maalum wa neno uliozoeleka. Katika mabadiliko ya lugha, irabu inaweza kuchopekwa baina ya konsonanti, au konsonanti inaweza kuchopekwa baina ya irabu, au hata kiyeyusho kuingizwa baina konsonanti. Aidha, konsonanti inaweza kuingizwa katikati ya irabu mbili na hivyo



kuleta mpangilio wa silabi wa asilia, na kuondoa mfuatano wa irabu mbili. Kutokana na utafiti huu, washiriki wa mawasiliano walikuwa wanachopeka sauti mpya katika baadhi mifumo ya maneno. Vilevile, baadhi ya maneno yalikuwa yakipoteza baadhi ya sauti ili kutosheleza mahitaji ya mabadiliko kama yalivyokuwa yanajitokeza. Hata hivyo, mbinu hii haikuonekana kupendelewa na watumiaji kwa kuwa utukizi wake ulikuwa nadra. Kwa mfano, jedwali hili linaonyesha jinsi washiriki wanavyochopeka na kupoteza sauti katika baadhi ya maneno.

**Jedwali 3**

Neno	Sauti iliyochopekwa	Sauti iliyopotea	Matokeo/fumo mpya
Bwana	/h/	/w/	Bhana
Acha	/h/	-	Hacha
Poa	/u/,/w/,/h/	-	pouwah
Noma	/u/	-	Nouma

Kutokana na jedwali hili, ni wazi kwamba watumiaji wa kitandazi wanadhahirisha mabadiliko ya mifumo ya maneno ya Kiswahili. Kuna kupoteza sauti kama vile katika neno [bwana] ambapo konsonanti /w/ imetoweka kabisa na badala yake konsonanti /h/ imechopekwa mahala pake. Katika mfumo mpya [hacha], tunatambua kwamba konsonanti /h/ imeingizwa mwanzoni mwa mfumo asilia [acha]. Kutokana na mabadiliko ya lugha, kadhia hii ni mpya kwa kuwa kaida iliyozeleka ni ya uchopekaji, na utowekaji/udondoshaji wa sauti katikati mwa mfumo wa neno. Wakati mwingine, watumiaji wa kitandazi wanachopeka sauti zaidi ya moja katika mfumo fulani wa neno kama katika neno [poa] ambapo sauti /u/, /w/ na /h/ zimeongezwa na kuzalisha mfumo mpya [pouwah]. Hii si hali ya kawaida katika mabadiliko ya lugha, hata hivyo, kwa kuwa sheria mpya zinajitokeza, ni vyema kuzielezea kikamilifu ili ziwe sehemu ya ufahamu na utafiti wa wanaisimu.

Kwa hiyo, kutokana na uchanganuzi wa jedwali hili, ni wazi kwamba mchakato wa uchopekaji umezoeleka miongoni mwa watumiaji wa kitandazi. Kuna baadhi ya maneno ambayo yanachukua zaidi ya sauti moja, na pia, kuna sauti ambazo zinaingizwa mwanzoni au mwishoni mwa neno. Ingawa kwamba baadhi ya maneno haya yamebadilika kimumo kwa kiwango kikubwa, ujumbe unaowasilishwa hauptei, hasa ikizingatiwa kwamba, maneno haya yangali katika muktadha na mahusiano ya kisemantiki na maneno mengine katika mawasiliano ya kitandazi. Aidha, wahusika wa kimawasiliano wanafahamu kiini cha mawasiliano, hivyo, ingawa baadhi ya sauti zinadondoshwa au kuongezwa, mawasiliano hayatatiziki kipragmatiki.

**Kubadilisha Sauti moja kwa nyingine**

Mbinu hii ya kubadilisha sauti moja kwa nyingine katika mawasiliano ya kitandazi inatumika sana ijapokuwa sio sauti nyingi zinaleta fahiwa ile ile. Ni sauti chache

ambazo zinapobadilishwa na msemaji au mwandishi hazibadilishi maana na dhamira ya msemaji. Kwa mfano jedwali hili linaelezea badiliko hili kwa mifano:

**Jedwali 4**

Neno	Sauti iliyobadilishwa	Sauti ya kawaida	Neno sanifu
Xawa Xana aixee	/x/	/s/	sawa
Xhemej yaixhe	/xh/	/ʃ/	Shemeji Yaishe
Bc	/c/	/s/, /i/	Basi
Bhana	/h/	/w/	Bwana

Katika jedwali hili, ruwaza kadha zinazuka: kwanza, katika mazingira ya kiisimu, konsonanti /s/ hubadilika na kuwa /x/, huku konsonanti /ʃ/ ikibadilika na kuwa sauti /xh/. Pili, ufupishaji kabisa wa baadhi ya sauti unatokea kwa namna kwamba sauti /c/ husimamia mkururo wa sauti /s/ na /i/ zinapofuatana katika fonolojia ya Kiswahili. Utamkaji wa ‘mfumo huu wa kiteknolojia’ unazingatia utamkaji wa konsonanti kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza’ yaani, kipasuo /b/ kinatamkwa kwa Kiswahili huku kitambaza /c/ kikitamkwa kwa lugha ya Kiingereza. Tatu, kiyeyusho /w/ kinadondoshwa na badala yake sauti /h/ inachopekwa pahala pale. Sababu moja kuu ya mchakato huu kutendeka ni kwamba, katika utamkaji wa kijamii, hasa mazungumzo ya mtaani, leksimu [bwana] ina kivuli chake kilichovuma, na ni rahisi kutamkwa [bana]. Kwa hiyo, leksimu-kivuli nyingine ya [bwana] inakuwa rahisi kushabihi [bana] kwa kutumia [bhana]. Dhana ya kutumia vifupishi kwa vipande vya kimofolojia tumevijadili katika sehemu inayofuata.

Mabadiliko ya lugha kama haya yamepata pingamizi tangu miaka mingi iliyopita. Njia mbalimbali ambazo wanajamii wametumia kupinga mabadiliko haya ni kupitia kwa uundaji wa taasisi na asasi mbalimbali za lugha kama vile TATAKI na CHAKITA, ambazo hulenga kufafanua namna ya kutumia lugha na sheria za kuelekeza wanajamii katika matumizi ya lugha. Kimsingi, vyombo hivi hudhamiria kudhibiti, kusimamisha au kubatilisha mabadiliko ya lugha. Hata hivyo, ni vyema kufahamu kwamba ingawa vyombo hivi, hata serikali ikiwemo, vinaweza kutumia nguvu na uwezo mkubwa wa kitaasisi, haviwezi kuelekeza watu namna ya kuzungumza wanapokuwa majumbani, mitaani, na baani na sehemu nyingine zisizosisitiza urasmi. Kwa kuwa sehemu hizi hazina urasimi wowote, na mabadiliko lugha hutokea katika sehemu hizi, basi ni wazi kwamba mabadiliko haya hayawezi kuzuiwa. Serikali mbalimbali duniani zimejaribu kudhibiti viwango na matumizi ya teknolojia mawasiliano, hasa zana za kusakura (*google, bing, yahoo*), blogu, *twitter, facebook* na kadhalika, hazijafanikiwa kabisa kwa kuwa hii ndiyo nduni bainifu ya jamii ya sasa. Maendeleo na matumizi ya teknolojia hizi katika jamii ya sasa ndiyo yanatawala mabadiliko ya lugha katika muktadha wa kisasa. Teknolojia ikizidi

kuwa na umaarufu kiuamilifu miongoni mwa wanajamii, basi lugha ya Kiswahili itazidi kuwa na mabadiliko kama haya tunayoshuhudia. Mara nyingi, tafiti mbalimbali za mabadiliko ya lugha hufanyika kidayakronia, muda mrefu baada ya mabadiliko hayo kukita mizizi lakini utafiti wa kisinkronia kama huu hauchangamkiwi sana kwa sababu ya kusubiri kuona kitakachotokea baada ya neno au sauti fulani kuingizwa katika lugha.

### **Hitimisho**

Mabadiliko ya lugha ni jmbo la kawaida na lisiloepukika katika kizazi chochote. Lugha ya Kiswahili kwa kuwa ni sehemu ya shani zinazobadilishwa na mambo kadha wa kadha, inadhihirisha mabadiliko haya katika mtagusano na teknolojia. Hakika, teknolojia ya kitandazi imekuwa na athari kubwa kwa lugha hii. Ingawa mabadiliko tuliyoshuhudia katika kazi yameegemea sana fonolojia, upo uwezekano kwamba fonolojia inaathiri mofolojia na mofolojia kuathiri semantiki ya mawasiliano ya kitandazi. Baadhi ya mabadiliko ya kifonolojia ambayo yalijadiliwa ni kama vile udondoshaji, uchopekaji wa sauti au mkururo wa sauti katika neno na pia ubadilishaji wa sauti badala ya nyingine. Utafiti mwingi zaidi wa kimofolojia unastahili kufanywa katika nyanja hii ili kuthmini mabadiliko yanayotokea.

### **Marejeleo**

- Aitchison, J. (2001). *Language Change: Progress or Decay?* 3<sup>rd</sup> edition. Cambridge: Cambridge University Press.
- Androutsopoulos, J. (2011). Language Change and digital media: a review of conceptions and evidence. In Coupland N. & Kristiansen, T. (Eds). *Standard languages and language standards in a changing Europe*. Oslo: Novus.
- Bakari, M. (1982). *The morphophonology of Kenyan Swahili dialects*. Unpublished PhD Dissertation. Nairobi: University of Nairobi.
- Bertoncini, Z.E. (2002). When grandfather came to life again: Said Ahmed Mohamed's new novel beyond realism. *Swahili Forum IX: 25-33*.
- Bynon, T. (1977). *Historical linguistics*. Cambridge: Cambridge University press. Cambridge University Press.
- Chiraghdin, S. & Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Oxford: Oxford University press.
- Crawley, T. (1992). *An Introduction to Historical Linguistics*. Oxford: Oxford University Press.
- Crystal, D. (2003). *English as global language*. 2<sup>nd</sup> ed. Oxford: Oxford University Press.
- Elms, D. (2013). *The relationship between language and culture*. Kayanora International exchange and language education center.
- Hickey, R. (2001). Language Change in Verschueren, J., Östman J., & Blommaert J. (eds.) *Handbook of pragmatics*. Amsterdam: John Benjamins
- Lewis, M.P. (2009). Language family trees in Indo-European: Ethnologue languages of the world. SIL International.
- Mey, J.L. (2009). *Concise encyclopedia of pragmatics*, 2<sup>nd</sup> ed. Oxford: Elsevier Ltd.
- Mgullu, R. S. (1999). Mtaala wa isimu: fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili. Nairobi: Longhorn.
- Milroy, J. & Milroy, L. (1985). Linguistic change, social network, and speaker innovation. *Journal of Linguistics 21: 339-384*.
- Mohamed, S.A. (2002). *Jicho la Ndani*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

- Njogu, K. na wenzake. (2007). *Sarufi ya Kiswahili: uchanganuzi na matumizi*. Nairobi : Jomo Kenyatta Foundation.
- Obuchi S. M. & Mukhwana A. (2015). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Shitemi, N.L. (2010). *Ushairi wa Kiswahili kabla ya karne ya ishirini*. Moi University: Moi University Press.
- Strazny, P. & Trask. R.L. (2000). *Dictionary of Historical & Comparative Linguistics*. 1<sup>st</sup> ed. New York: Routledge.
- Trask, R.L. (1994). *Language Change*. London: T.J. International Ltd.
- Trudgill, P. (1989). Contact and Isolation in Linguistic Change. In Breivik, L. E. & Jahr, E. H. (eds.) *Language change: Contributions to the study of its causes* (pp.227-237). Berlin: Mouton de Gruyter.
- Wardhaugh, R. (2002). *An introduction to Sociolinguistics* (4<sup>th</sup> ed.). Oxford: Blackwell Publishers.

